# Kipimo cha Haraka cha Antijeni (RAT)

## Jinsi ya kutumia vizuri kipimo cha haraka cha antijeni

**Kwa vipimo vyote vya haraka vya antijeni, unatakiwa wakati wote:**

- Kuangalia kuwa kipimo hakijaisha muda wake
- Kuosha au kusafisha mikono yako kabla na baada ya kufanya kipimo
- Kufuata kwa uangalifu maagizo ya kipimo yaliyoelezwa kwenye maelezo ya ufungaji



## Kitu ambacho unatakiwa kufanya na kutofanya



### Vipimo vinavyotumia kutema au mate

Dakika 30 kabla ya kufanya kipimo:



Usile



Usivute sigara



Usipige mswaki



Usitafune pipi mpira



Unapokaribia tu kufanya kipimo, kohoa kikohozi kikubwa mara 3 hadi 5 kwenye barakoa ya uso au tishu na ukiwa mbali na watu wengine.



### Vipimo vinavyotumia sampuli kutoka puani mwako



Puliza pua yako kabla ya kufanya kipimo.



Usiguse ncha laini ya kijiti kidogo, kinachojulikana kama usufi.

Kumbuka, kila kipimo kinaweza kutumiwa mara moja tu.





Kwa habari zaidi kuhusu upimaji wa haraka wa antijeni, piga simu kwenye

**National Coronavirus Helpline: 1800 020 080**

Chagua chaguo la 8 kwa usaidizi wa ukalimani bila malipo.

Unaweza pia kutembelea kwenye health.gov.au



Australian Government